

# MIELEKEO YA WANAFUNZI KUHUSU LUGHA YA KISWAHILI: MFANO WA MIKOA YA PWANI NA NYANZA, NCHINI KENYA

*E.S. Mohochi*

Idara ya Lugha na Isimu, Chuo Kikuu cha Egerton, Njoro, Kenya

## UTANGULIZI

Aghalabu binadamu, katika pilikapilika za maisha, huhitaji kufanya uchaguzi wa vitu, hali au mambo mbalimbali ili kufanikisha maisha yake. Ili kufanya uchaguzi huo, pana masuala mbalimbali muhimu ya kuzingatia, yakiwemo; mahitaji, matumaini na matarajio yake pamoja na vidadala vilivyopo. Mfano wa hali hii unadhihirika tunapotazama suala la lugha. Kama jamii fulani inazo lugha nyingi, lugha hizo hupata hadhi tofauti na hutumiwa katika mazingira tofauti. Hivyo, lugha moja au rejista zake zaweza kugawanywa na kutumiwa kutekeleza majukumu mbalimbali ya mawasiliano. Mgawanyo huo husababisha watumiaji kuzua mielekeo mbalimbali kuhusu lugha hizo, na hivyo basi kuathiri matumizi ya lugha hizo katika miktadha na nyanja tofauti, ikiwemo elimu.

Kwa muda mrefu pamekuwepo na imani kwamba wakaazi wa mikoa ya Pwani na Nyanza nchini Kenya, wana mielekeo tofauti kuhusu lugha ya Kiswahili. Gorman (1974) alisema kwamba wakaazi wa Pwani wana mielekeo chanya kwa lugha ya Kiswahili, ilhali wale wa Nyanza wana mielekeo hasi. Naye Odinga (1967) alisema kuwa jamii ya Waluo mkoani Nyanza, walijenga mielekeo hasi kwa lugha ya Kiswahili wakati wa utawala wa kikoloni kwa sababu ndiyo lugha iliyotumiwa na maaskari waliokuwa katili na wanyanyasaji. Mazrui (1981) anaeleza kwamba hadi sasa ukadiriaji wa mielekeo na tabia ya lugha kuhusu Kiswahili umetokana na hali ya kukisia tu.

Mazrui (1981) pamoja na Onyango (1990:14) wanang'ang'ania kuwa, maoni yanayotolewa kwamba jamii ya Waluo haipendi lugha ya Kiswahili ni madai ambayo hayana uthibitisho wowote. Katika misingi hiyo, ni muafaka kuyafanyia madai haya utafiti ili ukweli ubainike. Makala haya yanachangia hilo kwa kuripoti matokeo ya utafiti uliofanywa mwaka 2000 kupima mielekeo ya wanafunzi wa shule za upili kuhusu Kiswahili katika hiyo mikoa miwili nchini Kenya ili kuchangia uelewekaji wa hali ya mielekeo kwa Kiswahili.



## Dhana ya Mielekeo na Ujenzi wa Mielekeo

### *Dhana ya Mielekeo*

Dhana ya mielekeo imetumiwa na wanasaikolojia pamoja na wanaisimujamii wengi kwa muda mrefu kiasi kwamba ni sharti tutarajie mabadiliko katika uelewa na matumizi yake. Hata hivyo, maana ya kimsingi imesalia ileile (Triandis, 2: 1971). Pamoja na ukweli kuwa watu wengi sana wametoa mchango wao wa maelezo kuhusu dhana ya mielekeo; na wakatofautiana katika maelezo yao, yapo mambo ya msingi ambayo yanajitokeza katika maelezo yao wote. Kwa maana hiyo, wote wanakubaliana kuhusu mielekeo ni nini, japo wanaieleza kwa namna tofauti.

Mielekeo ni dhana ambayo imeshughulikiwa na wataalamu wengi mno. Edwards (1982) anakiri kuwa ingawa dhana hii imetanda kote katika taaluma ya saikolojia jamii, hakujapatikana makubaliano miongoni mwa wataalamu kuhusu kijejezi cha mielekeo. Ukweli kuwa dhana hii imeshughulikiwa na wataalamu wengi, ni dhihirisho la umuhimu wake katika maisha ya binadamu kwani ni nadra sana kwa watu kutumia muda wao mwingi kulitafiti na kulichunguza swala ambalo si muhimu na halichangii utatuzi wa matatizo yao na kuyaboresha maisha yao. Aidha, hali hii inatuonesha kuwa bado yapo masuala kadhaa yanayohusu mielekeo ambayo hayajawekwa bayana. Kwa hakika suala zima la mielekeo kuhusu lugha ya Kiswahili linahitaji kuwekwa dhahiri zaidi.

Msingi wa ufafanuzi wa mielekeo ni maelezo ya Allport (Kiesler et al., 1969:2) anayeieleza mielekeo ifuatavyo:

*mielekeo ni hali ya kuwa tayari kifika na kifahamu ambayo imeratibishwa kutokana na tajriba na inayotoa athari ya moja kwa moja au inayobadilika badilika kwa mwikio wa mtu kuhusu vitu vyote na hali zote zinazohusiana (tafsiri yetu).*

Jambo linalosisitizwa katika ufafanuzi wa mielekeo ni ile hali ya kuwa tayari kiakili (Agheyisi na Fishman, 1970). Kulingana na Oppenheim (1966:105), wakati wote binadamu huwa na mielekeo lakini katika hali bwete. Ipo akilini muda wote lakini inajitokeza na kubainika tu pale tunapokumbana na kitu fulani. Naye Sarnoff (Edwards 1985:139) anaeleza hali hiyo kama elekeo la kuonesha hisia za kupenda ama kutopenda kitu fulani.

Licha ya ukweli kwamba swala la mielekeo limo maishani mwetu, haijashughulikiwa kikamilifu katika taaluma ya Kiswahili. Wataalamu wachache ambao wamelitafiti ni pamoja na Onyango (1990), Okwany (1995) na Muzuni (1981). Bado kuna mambo mengi sana ambayo yanastahili kuchunguzwa na kuwekwa bayana.

**Muundo**  
Mielekeo  
ufahamu,  
1970; Op  
pamoja  
kawaida  
kisha hup

Sehe  
tunayoya  
zetu kuhu  
sana au  
uthabiti  
pembeni.  
kubadilish  
fulani (Tr  
akajenga  
hamu ya  
1982:20).

Sehe  
wetu mpa  
kwa chon  
kwanza h  
Baada ya  
wapo baa  
kuwa mit  
katika ku  
kinachotu  
kisichotuv

Sehe  
ufahamu  
ufahamu  
huonyesh  
chombo h

**Ujenzi na**  
Binadamu  
Tunajifun  
yanayotuz  
mielekeo  
zetu. Kwa



### **Muundo wa Mielekeo**

Mielekeo ina muundo unaojumlisha sehemu tatu muhimu ambazo ni sehemu za ufahamu, hisia, na vitendo (Allport, akinukuliwa na Mazrui 1981; Summers 1970; Oppenheim 1966; Lemon 1973; Ajzen na Fishbein 1980; Triandis 1971; pamoja na Edwards 1985). Edwards (1985:139) anasema kwamba, kwa kawaida mtu hupaswa kupata ufahamu na kujenga imani kuhusu kitu fulani, kisha hupata hisia za mwitikio; hali ambazo hudhihirisha matendo maalum.

Sehemu ya ufahamu au utambuzi inajumuisha mkusanyiko wa yale yote tunayoyafahamu kuhusu chombo cha mwelekeo. Suala muhimu hapa ni imani zetu kuhusu chombo hicho; imani ambazo zaweza kuwa na umuhimu mkubwa sana au mdogo. Kwa kawaida, imani za karibu humfanya mtu kudhihirisha uthabiti mkubwa katika mwelekeo wake, tofauti na zile imani ambazo ni za pembeni. Kutokana na mantiki hiyohiyo, inafahamika kwamba ni rahisi zaidi kubadilisha mwelekeo wa mtu iwapo imani zake hazina msingi katika swala fulani (Triandis, 1971:9). Kwa kawaida basi, mtu hupata utambuzi kuhusu kitu, akajenga hisia fulani kukihusu na kutokana na hayo akatenda ama kuonyesha hamu ya kutenda kwa namna maalum kuhusiana na kitu hicho (Edwards, 1982:20).

Sehemu ya pili ya mwelekeo ni sehemu ya hisia. Kutokana na ufahamu wetu mpana wa chombo maalum cha mwelekeo, huwa tunajenga hisia fulani kwa chombo hicho. Yale mafungo mbalimbali ya ufahamu katika sehemu ya kwanza huhusishwa na hali mbili tofauti; ama ya kufurahisha au ya kukasirisha. Baada ya muda, hili huibua ama hali chanya au hasi katika nafsi zetu. Aidha, wapo baadhi ya wataalamu, kama vile Peak (Triandis, 1971:11), anayesema kuwa mitazamo yetu kuhusu kitu chochote hutegemea nafasi ya chombo hicho katika kuyatekeleza malengo yetu. Tutakuwa na hisia za kupenda kile kinachotusaidia kuyafikia malengo yetu na hisia za kuchukua kile kisichotuwezesha kufanya hivyo.

Sehemu ya mwisho ya mwelekeo ni sehemu ya matendo. Baada ya kuwa na ufahamu mpana kuhusu kitu fulani, na kujenga hisia maalum kuambatana na ufahamu huo, tunadhihirisha hayo yote kwa matendo yetu. Matendo haya huonyeshwa waziwazi ama kwa kukiri kuwa tunaweza kuyatenda kuhusiana na chombo hicho.

### **Ujenzi na Ukuzaji wa Mielekeo**

Binadamu hawazaliwi na mielekeo waliyonayo kuhusu mambo mbalimbali. Tunajifunza mielekeo hiyo tunapohusiana na kutangamana katika mazingira yanayotuzunguka. Kulingana na Allport (Triandis, 1971:101), tumepata mielekeo mingi tuliyonayo kwa kuzungumza na familia zetu pamoja na marafiki zetu. Kwa maana hiyo, msingi wa mielekeo yetu ni mazungumzo baina yetu na



wenzetu. Zaidi ya familia, ni kawaida kwa binadamu kujiunga na vikundi mbalimbali. Mielekeo ya wanachama wa hivyo vikundi huathiri sana na kuongoza ukuaji wa mielekeo yetu. Kutokana na hali hii, utaona kwamba watu wengi sana wanaathiri mielekeo waliyonayo wanafunzi kuhusu lugha ya Kiswahili. Tunatarajia mieleko yao kuongozwa na mielekeo ya wazazi na jamaa wengine, walimu wao, pamoja na marafiki wanaohusiana nao. Katika mijadala yao shuleni, kama wanafunzi wengine hawaipendi lugha hii na wanaidharau, au walimu wanaizungumzia vibaya, basi hata wale ambao awali waliipenda wataweza kuanza kuwa na mawazo tofauti.

Mielekeo pia hujengwa kutokana na uhusiano wetu na chombo maalum cha mielekeo. Japo mielekeo ijengwayo kwa namna hii ni michache, huwa ya kati zaidi kwa mtu kuliko ile ijengwayo kutokana na athari kutoka kwa watu wengine. Itokeapo kwamba tajriba ya mahusiano yetu na chombo hicho ni mabaya yasiyofurahisha, mielekeo inayozuka huwa mizito sana. Kwa mfano, wapo watu wanaoshikilia imani kwamba Waswahili ni wajanja na wadanganyifu au Wakikuyu pamoja na Wachaga ni wezi na wakora. Mtu ambaye aliwahi kudanganywa na Mswahili au kuibiwa na Mchaga ama Mkikuyu ataweza kujenga mielekeo ya kudumu kuhusu makundi hayo ya watu. Tatizo ni kwamba tunafanya hivyo kwa kujumuisha bila kukumbuka kuwa ni Mswahili, Mchaga na Mkikuyu fulani aliyefanya hivyo wala si wote.

Ipo mitazamo ambayo hujengwa kwa minajili ya kuinga, kutetea na kuendeleza hisia za ubora wetu; yaani kuendeleza msimamo tunaouthamini. Triandis (1971) anatoa mfano wa mielekeo ya weupe kuwadharau weusi, ili waendeleo kujiona bora. Miongoni mwetu pia tuna tabia ya kuyadharua makabila mengine kwa kutoa vijisababu visivyo na msingi, mradi tujione bora. Vivyohivyo, wapo wanafunzi wengi sana katika shule za upili pamoja na vyuoni ambao daima huzungumza Kiingereza na kuepuka matumizi ya Kiswahili ili wajiweke katika kundi bora ambalo ni tofauti na lile la kawaida. Wanapotumia Kiswahili wanakitumia kwa kukichanganya na Kiingereza. Watu kama hawa huwa wamejenga na kukomaza mielekeo ya kukipendelea Kiingereza na kukidumaza Kiswahili.

Kwa jumla binadamu hujenga mielekeo chanya kwa chombo ambacho kinampa manufaa fulani na mielekeo hasi kwa kile ambacho hakioneshi manufaa yoyote kwake. Manufaa haya hujitokeza katika hali nyingi na tofauti sana. Yanaweza kujitokeza kwa kupata alama "A" katika mtihani, kupongezwa na wenzako, kushinda katika mjadala na kadhalika.

### **Mielekeo Kuhusu Lugha**

Japo mielekeo ni kipengele ambacho kimefanyiwa utafiti sana, hasa kuhusu mahusiano ya kikabila na imani za kisiasa, mielekeo ya lugha ni eneo ambalo

halijashug  
mkubwa s  
wa taalum  
kuwa mie  
wataalamu  
Fasold 19  
Carranza  
awali za r  
kwa upan  
mwitikio  
wanasema

Ka  
ka  
ha  
ma  
kij  
hu  
ju

Hali  
mfano, w  
kama lugh  
muhimu y  
waliochuk  
zikachuku  
Kenya na  
bali matur  
zile zinaz  
katika jam

Miele  
lugha pan  
anasema l  
utafiti mp  
na tofauti  
sarufi. Hi  
taaluma  
mielekeo

Mion  
pamoja r



halijashughulikiwa sana. Hata hivyo, eneo hili limeanza kupewa umuhimu mkubwa sana katika miaka ya karibuni na limechangia sana katika uendelezaji wa taaluma ya isimujamii (Carranza, 1982). Carranza (1982) anaendelea kusema kuwa mielekeo ya lugha ni mada ya isimujamii ambayo imetafitiwa na wataalamu mashuhuri, wakiwemo; Cooper 1974, 1975b, pamoja na Shuy na Fasold 1973. Pamoja na ukweli huo, akiwanukuu Agheyisi na Fishman, Carranza (1982) anaendelea kueleza kuwa mada hii bado iko katika hatua za awali za makuzi yake. Kulingana na Ryan et al. (1982:7), mielekeo ya lugha, kwa upana wake ni ukadiriaji wowote wa kihisia, kiufahamu, na kitabia, wa mwikitio wetu kwa lugha tofauti au wazungumzaji wake. Kwingineko, wanasema:

*Katika kila jamii, nguvu tofauti za makundi mbalimbali hudhihirika katika namna tofauti za matumizi ya lugha na katika mielekeo kuhusu hayo matumizi tofauti. Kwa kawaida, kundi lenye nguvu huendeleza matumizi yake ya lugha kama bora na yanayohitajika ili kujiendeleza kijamii. Matumizi ya lugha, lahaja ama lafudhi ya hadhi ya chini hupunguzia watu wa kundi nyonge nafasi za mafanikio katika jamii kwa jumla (Ryan et al., 1982: 1).*

Hali hii kwa jumla huathiri sana matumizi ya lugha katika jamii. Kwa mfano, wakati wa ukoloni, Waafrika wengi walizitazama lugha za wakoloni kama lugha bora na ikawabidi kujifunza na kuanza kuzitumia kama namna moja muhimu ya kujiendeleza na kupanda hadhi. Baada ya uhuru kupatikana, wale waliochukua hatamu za uongozi wakawa wanazitumia lugha hizo, na hivyo zikachukuliwa kuwa kielelezo cha lugha muafaka. Kwa hakika, hali yetu nchini Kenya na nchi nyingine za Kiafrika, swala si matumizi tofauti ya lugha moja bali matumizi, na hadhi tofauti za lugha mbalimbali. Zipo lugha zinazobezwa na zile zinazotukuzwa kwa sababu zinanasibishwa na wanyonge na wenye nguvu katika jamii katika mfuatano huo.

Mielekeo ya lugha hujumuisha umuhimu wa kijamii tunaouambatanisha na lugha pamoja na namna tofauti za matumizi ya lugha katika jamii. Ryan (1982), anasema kuwa namna tofauti za matumizi ya lugha ambazo zimekwishafanyiwa utafiti mpana ni: lugha tofauti, lahaja za kikabila, kijamii, na kimaeneo; pamoja na tofauti nyingine za kiisimu kama vile matamshi, uteuzi wa msamiati na sarufi. Hizi tafiti zote zinadhihirisha umuhimu wa swala la mielekeo katika taaluma ya isimu. Licha ya umuhimu huo, hali mbalimbali kuhusiana na mielekeo ya lugha ya Kiswahili hazijafanyiwa utafiti wa kutosha.

Miongoni mwa mambo ya msingi yanayochangia mielekeo ya lugha ni pamoja na umuhimu wa lugha husika (Ryan et al., 1982). Aidha, lugha



inapotumiwa na watu wengi katika shughuli nyingi na muhimu, watu huipa umuhimu na kujenga mielekeo chanya kwake. Kulingana na Fishman (Ryan et al., 1982:4), hadhi ya lugha hupanda na kushuka kulingana na wingi pamoja na umuhimu wa majukumu ya kiishara inayoyatekeleza. Naye Edwards (1982:32) anasema kuwa kwa kawaida, lugha iliyo na hadhi ya juu na ambayo imepata maenezi mapana, itakuwa na mielekeo tofauti inapolinganishwa na mielekeo ya lugha nyingine ndogo. Licha ya hadhi, umuhimu wa lugha huchangiwa pia na wazungumzaji, na asasi zinazoiunga mkono. Hadhi ya lugha hujumuisha nguvu za kiuchumi, kijamii na kisiasa walizonazo wazungumzaji wake. Upande wa wazungumzaji unahusu idadi ya wazungumzaji wake, ilhali la muhimu kuhusu asasi ni kiasi cha kukubalika na matumizi yake kama lugha rasmi katika asasi hizo (Ryan et al., 1982). Asasi muhimu hapa ni pamoja na matumizi yake katika viwango mbalimbali vya elimu; idara kadhaa muhimu za serikali za kitaifa, pamoja na zile za kimaeneo; na matumizi yake katika shughuli za kibiashara, uchapishaji, na vyombo vya habari.

Sababu nyingine inayosababisha mielekeo tofauti kuhusu lugha mbalimbali ni yale majukumu mbalimbali ambayo lugha hizo huwa zimekabidhiwa na jamii. Lugha inapopewa majukumu ya msingi katika jamii, watumiaji wake huipa hadhi na matokeo yake ni kuwa jamii kwa jumla huithamini na kuwa na mielekeo bora kuihusu. Tofauti na hali hiyo, lugha inayotekeleza majukumu ya yasiyo na umuhimu mkubwa hudharauliwa na kubezwa.

Utafiti juu ya mtazamo wa watu kuhusu lugha tofauti umedhihirisha kuwa madai kwamba lugha hupendelewa kwa sababu ni bora kuliko nyingine ama ina ujumi mzuri hayana mashiko. Katika mizani ya kiisimu, hakuna lugha iliyo bora kuliko nyingine (Trudgil 1974; Edwards 1982; Bourhis 1982). Akilieleza hoja hiyo zaidi, Edwards (1982:21), anakiri kwamba tathmini ya lugha, lahaja, lafudhi au matamshi haijikiti sana katika ubora au ujumi wa lugha husika bali hutokana na hali ya kuipendelea lugha hiyo; hali ambayo inatokana na mazoea, na imani ya jamii kuhusu hadhi na staha ya lugha hiyo pamoja na wazungumzaji wake. Naye Trudgil (1974:8-9) anasema kuwa tathmini zinazohusu usahihi na usafi wa lugha si za kiisimu bali ni za kijamii.

Morocco, Tunisia na Algeria ni mataifa ambayo yalikuwa na lugha moja iliyoenea kwa mapana na marefu hata kabla ya ukoloni wa Mfaransa. Lugha ya Kiarabu ilikuwa imefaulu kuibuka kama lugha jumuishi na kuchukua mahali pa lugha nyingine mbalimbali za kienyeji. Hata hivyo, sera za Mfaransa zilivunjesha lugha ya Kifaransa kupata hadhi ya juu, na kuzua hali ya uwili-lugha miungoni mwa wengi. Pamoja na jitihada za muda mrefu za kuhimiza matumizi zaidi ya Kiarabu kama hapo awali, jitihada ambazo pia zimeoanishwa na suala la dini ya Kiislamu, bado wapo watu wengi, hasa wasomi, ambao wanapendelea ufahamu wao wa Kifaransa. Hali hii, kwa kiwango kikubwa,



hutokea kwa sababu ya umuhimu mkubwa ambao tumekubali kuzipa lugha hizi za kigeni. Bourhis (1982: 44-45) anasema:

*... hadi leo ufahamu wa Kiarabu sanifu ni silaha muhimu imwezeshayo mtu kupata kazi katika serikali, elimu, pamoja na sekta ya biashara huko Afrika Kaskazini.*

Afrika Mashariki tuna lugha ya Kiswahili ambayo inajulikana na wengi. Pia inajulikana katika sehemu nyingi za Afrika ya Kati na sehemu nyingine za ulimwengu. Licha ya kuwa na amali hiyo, sisi pia tumeruhusu lugha ya Kiingereza kuyatawala maisha yetu, na kama ilivyo huko Afrika Kaskazini, ufahamu wa lugha ya Kiingereza hapa kwetu umechukuliwa kuwa silaha muhimu katika mapambano kazini. Wakati ambapo Kiarabu kinachukua mahali pa Kifaransa, hatua kwa hatua, katika elimu ya msingi na sekondari huko Afrika Kaskazini, Kifaransa kimeendelea kuwa lugha ya elimu ya juu na vyuo vikuu (Gordon, Bourhis 1982). Mafanikio baina ya Kenya, Uganda, na Tanzania katika kuipa lugha ya Kiswahili nafasi zaidi yanatofautiana sana. Japo tumejaribu kuipa nafasi zaidi katika elimu ya msingi na ya sekondari, hali hii haijitokezi katika elimu ya juu, ikiwa ni pamoja na ile ya vyuo vikuu.

Kwa hakika mtazamo wetu wa lugha unasikitisha na unapaswa kuchunguzwa upya. Wakati ambapo Waarabu wa Tunisia, Morocco, na Algeria wanazidi kujivunia Kifaransa, huko nchini Ufaransa kwenyewe, matamshi yao ya lugha hiyo yanadharauliwa sana (Bourhis 1982). Vivyo hivyo, Kiingereza tunachokitumia sisi hapa Afrika Mashariki na sehemu nyingine za Afrika ndicho kinachodharauliwa na kuonwa cha chini zaidi kinapolinganishwa na Kiingereza kitumikacho Uingereza na sehemu nyingine.

Yaliyotokea huko Kusini Mashariki mwa Asia yanaweza kuwa mfano wa kuigwa ili kuirekebisha hali yetu katika eneo la Afrika Mashariki. Mataifa ya Cambodia, Laos, na Vietnam yaliipokea lugha ya Kifaransa kama ilivyokuwa katika sehemu nyingine zilizoathiriwa na Ufaransa, lakini hawakuziacha mbali lugha zao. Cambodia na Laos walitumia Kifaransa pamoja na Laotian na Khmer kama lugha zao za taifa. Baada ya muda wa harakati za kitaifa za ukombozi, lugha zao zilipata umuhimu zaidi na athari ya Kifaransa ikaanza kudidimia. Bourhis (1982:47) anaiweka hali hiyo bayana:

*...ikilinganishwa na lugha zao za kitaifa, Kifaransa hivi sasa kina umuhimu tu kutokana na hadhi yake ya lugha ya kigeni iliyo na umuhimu katika mawasiliano ya kimataifa. Kimsingi, Kusini Mashariki mwa Asia ndiyo sehemu moja ambapo Kifaransa kimepoteza umuhimu wake kama*



*lugha ya mawasiliano miongoni mwa wasomi na idadi kubwa ya watu wengine.*

Funzo muhimu tunalolipata hapa ni kuwa inawezekana kutupilia mbali kasumba ya kuziamini na kuziabudu lugha za kigeni huku tukizibeza lugha zilizotukuza. Tunao uwezo wa kubadili hali ya lugha hapa nchini kwa kukipatia Kiswahili nafasi zaidi na kupunguza nguvu za Kiingereza.

Nchi nyingi za Afrika, ambazo zilikuwa matokeo ya uamuzi wa wakoloni ambao hawakujali asili za watu wakati wa kuweka mipaka, zinajumuisha watu wanaozungumza lugha nyingi tofautitofauti. Wanaisimu mbalimbali wanakadiria kuwa barani Afrika kunazungumzwa lugha na lahaja kati ya 800 na 1,140 (Bourhis 1982). Katika hali kama hiyo ya wingi wa lugha katika mataifa ya Afrika, ilibidi iteuliwe lugha itakayotumiwa kujenga mataifa huru. Kutokana na wingi wa lugha, ikawa rahisi kwa nchi nyingi kuchagua lugha za wakoloni waliowatawala ili kuepuka uhasama wa kikabila ambao ungezushwa na uteuzi wa lugha moja badala ya nyingine. Aidha, lugha hizo zilidhaniwa kuwa muafaka kwa maendeleo ya kiteknolojia na mawasiliano ya kimataifa. Uteuzi huu wa Kifaransa, Kiingereza na lugha nyingine za kikoloni uliathiri sana mitazamo yetu ya lugha na kuchangia mielekeo ya lugha tunayoipata sasa barani Afrika. Lugha hizi zilipata hadhi maalum na zikapendelewa na watu ambao wakati huohuo walijenga mielekeo hasi kwa lugha za kiasili.

Wasomi wengi wa Afrika, ambao wamepata elimu kwa kutumia lugha mbalimbali za kikoloni wamekuwa mstari wa mbele kutetea nafasi nzuri za lugha hizo katika nchi zao tofautitofauti. Pamoja na hizo jitihada zao za kibinafsi, lugha hizo zimesalia kuwa za watu wachache sana. Akizungumza kuhusu lugha ya Kifaransa katika nchi za Afrika, Bourhis (1982:49) anasema yafuatayo:

*Licha ya kuungwa mkono na taasisi kadhaa katika elimu, serikali, biashara na vyombo vya habari, Kifaransa ni lugha inayojulikana na wachache ambao wamepitia elimu ya kimagharibi na ambao wanapata manufaa kutokana na hatua ya kuendelea kuipa lugha hiyo hadhi ya juu katika mataifa hayo. Hadi sasa, wasomi wengi katika nchi za Afrika wanaamini lugha ya Kifaransa na ustaarabu wa Ufaransa ni bora kuliko lugha na utamaduni wa Mwafrika, na hutetea matumizi ya lugha hiyo katika maswala ya kiulimwengu kama yale ya umoja wa mataifa.*

Hali hii inapatikana vilvile katika nchi zinazozungumza Kiingereza. Matokeo ya hali hiyo ni kuwa watu wengi wanajenga mielekeo hasi kuhusu lugha zao za kiasili. Tukizingatia nafasi waliyonayo wasomi ya kuongoza dira



ya maamuzi ya serikali pamoja na athari yao kubwa kwa umma ambao unawaheshimu na kuwaenzi ni wazi kwamba wao ni maadui wakubwa wa lugha za Kiafrika. Onyango (1990), kwa mfano, anasema kuwa kwa kiwango kikubwa wasomi nchini Kenya hupendelea matumizi ya lugha ya Kiingereza katika shughuli zote muhimu. Je, wanafunzi katika mikoa ya Pwani na Nyanza nchini Kenya wana mielekeo gani kuhusu lugha ya Kiswahili?

### **Mielekeo ya Wanafunzi Kuhusu Kiswahili Mikoani Pwani na Nyanza**

Utafiti huu ulifanyika mwaka wa 2000 katika hiyo mikoa miwili ya nchi ya Kenya. Madhumuni ya misingi ya utafiti yalikuwa ni kutambua mielekeo ya wanafunzi kuhusu lugha hii, hasa tukikumbuka kuwa kwa muda mrefu imesemekana kwamba watu katika mikoa hii wana mielekeo tofauti kuhusu lugha ya Kiswahili. Kabla ya kuripoti matokeo ya utafiti huu, tutaeleza kwa muhtasari mbinu zilizotumika katika utafiti huu.

### **Mbinu za Utafiti**

Utafiti huu ulifanyika mwaka wa 2000, wasailiwa walengwa wakiwa wanafunzi wote wa kidato cha nne katika mikoa ya Nyanza na Pwani mwaka huo. Sababu za uteuzi wa mikoa ya Nyanza na Pwani ni tetesi za muda mrefu kwamba wakaazi wa mikoa hiyo miwili wana mielekeo inayotofautiana kuhusu lugha ya Kiswahili (Gorman 1974; Odinga 1969; Mazrui 1981; na Onyango 1990). Kwa sababu ya wingi, ilitibi kufanyike uteuzi wa shule na wanafunzi wa kushiriki.

Mbinu ya uteuzi nasibu ilitumika kuteua shule 14; 7 kutoka kwa kila mkoa. Madhumuni ya awali yalikuwa kuitumia mbinu hiyo kuchagua wanafunzi 20 kwa kila shule ili tupate jumla ya washiriki 280. Hata hivyo, kwa sababu tofauti katika shule mbalimbali idadi kamili ya wanafunzi walioshiriki ilikuwa 278 (138 Nyanza na 140 Pwani).

Data kuhusu mielekeo ya wanafunzi ilikusanywa kwa kutumia hojaji iliyoandaliwa kufuatia mfumo wa Likert. Baada ya kupitia vitabu na machapisho mengine mbalimbali kuhusu swala la mielekeo ya lugha nilikusanya kauli 33 ambazo zilijumuishwa kuunda hojaji ya Likert. Baada ya utafiti wa awali nyanjani, hojaji hii ilirekebishwa. Kauli 20 kati ya zile 33 za awali ndizo zilihifadhiwa kuunda hojaji ambayo ilitumika katika utafiti wenyewe. Uteuzi wa kauli za kudondoshwa na zile za kubakizwa ulifanywa kulingana na utaratibu unaoelezwa na Lemon (1973). Utaratibu huo unapendekeza kufanywa uchunguzi wa kauli nyingi na kuteua zile ambazo zinaonesha tofauti kubwa zaidi kati ya asilimia 25% ya wale walio na mielekeo chanya na asilimia 25% ya



wale walio na mielekeo hasi. Kila moja kati ya zile kauli 33 za awali zilichunguzwa kwa utaratibu huu na 13 zikadondolewa.

Majibu yaliyotolewa kwa kauli hizo yalipewa alama kulingana na mfumo wa Likert (Jahoda na Warren, 1966). Kulingana na mfumo huo, majibu huoneshwa kwa kutumia vidadala vitano vinavyoeleza kiwango cha kukubaliana ama kutokubaliana na kauli fulani. Vidadala hivyo hupewa alama 1-5. Katika utafiti huu, vidadala vifuatavyo na alama zilizoonyeshwa vilitumika kwa kauli chanya kuhusu Kiswahili; nakubali kabisa(5), nakubali(4), sina hakika(3), sikubali(2) na sikubali kabisa(1). Mfumo huu wa kupeana alama uligeuzwa kwa kauli hasi. Jumla ya alama kutokana na majibu ya maswali yote inaashiria mielekeo aliyonayo mshiriki kuhusu lugha ya Kiswahili. Alama 60 itaashiria kwamba msailiwa haegemei upande wowote. Walio na zaidi ya alama 60 watakuwa na mielekeo chanya, ilhali msailiwa anayepata chini ya alama 60 atachukuliwa kuwa na mielekeo hasi kuhusu lugha ya Kiswahili.

### **Matokeo Ya Utafiti**

#### ***Mielekeo ya Wanafunzi Mkoa wa Nyanza***

<b>Shule</b>	<b>Alama za wastani</b>
1	84.35
2	81.38
3	82.14
4	79.3
5	79.84
6	82.04
7	87.2

**Alama Sawazishi Mkoani Nyanza = 82.32**

#### ***Mielekeo ya Wanafunzi Mkoani Pwani***

<b>Shule</b>	<b>Alama Sawazishi</b>
1	83.6
2	79.8
3	75.7
4	76.1
5	84.4
6	75.7
7	80

**Alama Sawazishi Mkoani Pwani =79.32**

Kutokana  
hojaji iliyot

1. Wa  
mie
2. Kur  
mik

Matokeo ha

1. Kinyur  
hawadl  
ya kaw
2. Ni waz  
katika  
umuhin  
huo.
3. Yaelek  
ya Kisv

Kuna kaul  
msimamo  
kupewa nch

1. Kiswahil

**MKOA**

**NYANZ**

**COAST**

**JUMLA**

Majibu  
kama som  
walipinga.

2. Ningepe

**MKOA**

**NYANZ**

**COAST**

**JUMLA**



za awali

na mfumo

2, majibu

kubaliana

5. Katika

wa kauli

hakika(3),

zwa kwa

naashiria

taashiria

lama 60

lama 60

ani

Kutokana na uchunguzi wa majibu ya wasailiwa kwa maswali funge katika hojaji iliyotumika ya mfumo wa Likert, yafuatayo yamebainika:

1. Wanafunzi katika mikoa yote miwili, Pwani na Nyanza, wamedhihirisha mielekeo chanya kuhusu lugha ya Kiswahili.
2. Kuna tofauti ndogo sana katika mielekeo ya wanafunzi katika hiyo mikoa miwili. (Nyanza-82.32 na Pwani-79.32).

Matokeo hayo yanatuongoza kutoa kauli muhimu zifuatazo:

1. Kinyume na imani ya muda mrefu, wanafunzi wa mkoa wa Nyanza hawadhihirishi mielekeo hasi kuhusu lugha ya Kiswahili iliyodhaniwa kuwa ya kawaida mkoani humo.
2. Ni wazi kuwa hiyo si sababu ya matokeo mabaya ya mtihani wa Kiswahili katika mkoa huo kama ilivyokisiwa na wengi. Hili linamaanisha kuwa kuna umuhimu wa kuendelea kutafuta sababu ya matokeo mabaya katika mtihani huo.
3. Yaelekea kwamba wanafunzi wa mkoa wa Pwani ndio hawaonyeshi hamu ya Kiswahili kama wenzao wa Nyanza, japo tofauti ni ndogo mno.

Kuna kauli mbalimbali katika hojaji ambazo ziliwataka wanafunzi kueleza msimamo wao kuhusu nafasi na hadhi ambayo lugha ya Kiswahili yapaswa kupewa nchini Kenya. Ifuatayo ndiyo ruwaza ya majibu yao kwa kauli hizo:

1. *Kiswahili Hakipaswi Kufundishwa Kama Somo la Lazima Katika Elimu.*

MKOA	MAJIBU CHANYA	MAJIBU HASI	WASIO NA HAKIKA	JUMLA
NYANZA	114	23	0	137
COAST	117	21	1	139
JUMLA	231	44	1	276

Majibu haya yanaonesha kuwa wengi wanapendelea Kiswahili kufundishwa kama somo la lazima. Asilimia 83.6% walipendelea hivyo na ilhali 15.9% walipinga. Tofauti baina ya mikoa haikuwa muhimu.

2. *Ningependa kuendelea kusoma Kiswahili baada ya kidato cha nne.*

MKOA	MAJIBU CHANYA	MAJIBU HASI	WASIO NA HAKIKA	JUMLA
NYANZA	111	10	16	137
COAST	85	19	36	140
JUMLA	196	29	52	277



Wanafunzi wengi zaidi (70.7%) walionyesha hamu ya kutaka kuendelea kusoma Kiswahili baada ya kidato cha nne ukilinganisha na 10.4% ambao hawana hamu hiyo, na 18.7% ambao hawakuwa na msimamo. Hata hivyo, kuna tofauti muhimu kati ya hiyo mikoa miwili. Wengi walikuwa na hamu hiyo mkoani Nyanza (idadi ni 111), kuliko Pwani (idadi: 85). Aidha, wakosa msimamo walikuwa wengi Pwani (idadi: 36) kwa kulinganisha na Nyanza (idadi:16).

3. *Napinga mpango wa matumizi ya Kiswahili kama lugha ya kufundishia masomo mengine nchini Kenya.*
4. *Twapaswa kufanya mpango wa kuanza kutumia Kiswahili kufundishia masomo mengine.*

MKOA	MAJIBU CHANYA	MAJIBU HASI	WASIO NA HAKIKA	MAJIBU KINZANI	JUMLA
NYANZA	54	23	3	57	137
COAST	36	50	4	50	140
<b>JUMLA</b>	<b>90</b>	<b>73</b>	<b>7</b>	<b>107</b>	<b>277</b>

Hizi kauli mbili (3&4) zimenuiwa kueleza kitu kimoja lakini zimewasilishwa kwa namna tofauti. Ya kwanza imewasilishwa kwa hali hasi ilhali ya pili ni chanya. Hali hii ni ya kawaida katika utafiti wa mielekeo kwani husaidia kuepuka wasailiwa wanaoamua kuchagua aina moja ya jibu bila kuzingatia kinachoulizwa katika kauli mbalimbali. Kwa sababu hiyo tunazichanganua pamoja. Maoni chanya ni mengi (90) kuliko hasi (73). Wanafunzi wengi zaidi mkoani Nyanza wanataka Kiswahili kitumike kufundishia kuliko Pwani. Hata hivyo, wengi zaidi (38.62%) walitoa majibu kinzani kuliko chanya (32.49%) na hasi (26.62%).

5. *Ni muhimu wageni wote wanaotaka kufanya kazi hapa nchini wajifunze Kiswahili.*

MKOA	MAJIBU CHANYA	MAJIBU HASI	WASIO NA HAKIKA	JUMLA
NYANZA	111	15	9	135
COAST	116	17	7	140
<b>JUMLA</b>	<b>227</b>	<b>32</b>	<b>16</b>	<b>275</b>

Kauli h  
Asilimia 82  
haikuwa na  
111 waliung  
hawakuwa r

6. *Lugha ya  
nchini Keny*

MKOA
NYANZA
COAST
<b>JUMLA</b>

Idadi k  
vyuo vya e  
Nyanza am  
87.3% wa  
msimamo.

7. *Nikiamu*

MKOA
NYANZA
COAST
<b>JUMLA</b>

Kuna majil  
wakati 18.1  
ya wanafu  
walikuwa  
wachache  
na Pwani.



Kauli hii inaungwa mkono na wengi sana katika mikoa yote miwili. Asilimia 82% ya wasailiwa inaunga mkono, 11.6% inapinga ilhali 5.8% haikuwa na msimamo. Matokeo yanaelekea kufanana katika hii mikoa miwili. 111 waliunga mkono Nyanza na 116 Pwani. 15 walipinga Nyanza, 17 Pwani. 9 hawakuwa na msimamo Nyanza, na 7 Pwani.

6. *Lugha ya Kiswahili yapaswa kufunzwa katika vyuo vyote vya elimu ya juu nchini Kenya.*

MKOA	MAJIBU CHANYA	MAJIBU HASI	WASIO NA HAKIKA	JUMLA
NYANZA	125	08	4	137
COAST	117	18	5	140
<b>JUMLA</b>	<b>242</b>	<b>26</b>	<b>9</b>	<b>277</b>

Idadi kubwa ya wanafunzi iko radhi kuendelea kusoma Kiswahili katika vyuo vya elimu ya juu. Majibu ni karibu sawa katika mikoa yote isipokuwa Nyanza ambayo ina wengi zaidi waliokuwa na msimamo chanya. Kwa jumla, 87.3% wanapendelea, 9.3% hawapendelei, na 3.2% tu ndio waliokosa msimamo.

7. *Nikiamua kuwa mwalimu nitafurahi sana kufundisha lugha ya Kiswahili.*

MKOA	MAJIBU CHANYA	MAJIBU HASI	WASIO NA HAKIKA	JUMLA
NYANZA	97	20	20	137
COAST	85	30	24	139
<b>JUMLA</b>	<b>182</b>	<b>50</b>	<b>44</b>	<b>276</b>

Kuna majibu chanya kuliko hasi katika mikoa yote miwili. 65.9% walikubali, wakati 18.1% walikataa. Aidha ni wazi kwamba kulikuwa na idadi kubwa sana ya wanafunzi waliokosa msimamo (44) ambayo ni asilimia 15.9%. Wengi walikuwa na msimamo chanya, wachache hasi na walikuwepo wengine wachache wasiokuwa na msimamo wowote mkoani Nyanza, unapolinganishwa na Pwani.



8. *Hakuna haja ya kutumia pesa za umma kuiendeleza lugha ya Kiswahili.*

MKOA	MAJIBU CHANYA	MAJIBU HASI	WASIO NA HAKIKA	JUMLA
NYANZA	117	16	4	137
COAST	112	13	15	140
<b>JUMLA</b>	<b>229</b>	<b>29</b>	<b>19</b>	<b>277</b>

Kutokana na majibu ya swali hili ni wazi kuwa wanafunzi wengi wangependa fedha nyingi zaidi za umma zitumike kuikuza lugha ya Kiswahili. Mahsusi 82.6% wanataka mali ya umma itumike kukuza Kiswahili, 10.4% hawataki, na 6.8% hawana hakika.

9. *Nina hamu ya kufanya mtihani ili nijiondolee usumbufu wa kujifunza lugha ambayo haitanisaidia baada ya elimu yangu.*

MKOA	MAJIBU CHANYA	MAJIBU HASI	WASIO NA HAKIKA	JUMLA
NYANZA	123	12	1	136
COAST	116	16	7	139
<b>JUMLA</b>	<b>239</b>	<b>28</b>	<b>8</b>	<b>275</b>

Wasailiwa wengi hawaoni kusoma Kiswahili kama bughudha ambayo wangependa kuepukana nayo mara tu baada ya mtihani wao. 86.9% hawabughudhiwi na elimu ya Kiswahili, 10.1% waliiona kama bughudha, ilhali 2.9% ndio hawakuwa na hakika.

10. *Idhaa zote za redio na televisheni zinazosajiliwa zapaswa kuwa na asilimia maalum ya vipindi vya Kiswahili.*

MKOA	MAJIBU CHANYA	MAJIBU HASI	WASIO NA HAKIKA	JUMLA
NYANZA	116	15	6	137
COAST	119	16	5	140
<b>JUMLA</b>	<b>235</b>	<b>31</b>	<b>11</b>	<b>277</b>

Majibu kwa kauli hii yanaonyesha kuwa wanafunzi wengi wangependa kusikiliza na kutazama vipindi vingi zaidi vya Kiswahili katika vyombo vya habari vilivyomo nchini Kenya. 84.8% wanapendelea matumizi zaidi ya

Kiswahili  
hawana

11. Ma  
Kiswahili

MK

NYA

COA

JUM

Ku  
wengi v  
Muung  
wakawa  
Ma  
wa mie  
kutoka  
nyingi y  
ya jumla  
zaidi ku  
sana ar  
kugundu  
vyombo  
katika e  
kusoma  
siku za

Hitimis  
Makala  
yametu  
mieleke  
ikiwa ni  
mbalim  
pamoja  
haswa k  
makala  
zilizotur  
utafiti h



Kiswahili katika vyombo vya habari, 11.1% hawapendelei, na 3.9% tu ndio hawana msimamo kuhusu swala hilo.

*II. Muungano wa mataifa ya Afrika mashariki wapaswa kuiteua lugha ya Kiswahili kutumika kuendesha shughuli zake rasmi.*

MKOA	MAJIBU CHANYA	MAJIBU HASI	WASIO NA HAKIKA	JUMLA
NYANZA	107	19	11	137
COAST	105	18	17	140
JUMLA	212	37	28	277

Kulingana na mwamko mpya wa umuhimu wa kushirikiana, wasailiwa wengi wanapendelea matumizi zaidi ya lugha ya Kiswahili kama lugha rasmi ya Muungano wa Afrika. 76.5% walisema hivyo, 13.3% wakakataa na 10.1% wakawa hawana msimamo maalum.

Majibu yaliyotolewa kwa hizi kauli zote yanaoana na uchunguzi wa jumla wa mielekeo ya wanafunzi katika hii mkoa miwili. Kwa mfano, wanafunzi kutoka mkoani Nyanza wanaelekea kuwa na msimamo chanya zaidi katika nyingi ya kauli zilizochunguzwa. Hali hii inakubaliana na matokeo ya mielekeo ya jumla kwani tuliona kwamba wanafunzi wa mkoa huu wana mielekeo chanya zaidi kuliko wenzao wa Pwani japo tofauti si kubwa sana. Hizi ni kauli muhimu sana ambazo zinaonesha nafasi ya Kiswahili nchini Kenya. Inatia moyo kugundua kuwa hawa chipukizi wangependa lugha hii ipewe nafasi zaidi katika vyombo vya habari, elimu, pia iwe na hadhi ya lugha rasmi si tu nchini, bali pia katika eneo la Afrika Mashariki. Wapo pia wale ambao wako tayari kuendelea kusoma lugha ya Kiswahili katika elimu yao ya juu. Bila shaka kuna matumaini siku za usoni.

#### **Hitimisho**

Makala haya yametufafanulia mambo kadha wa kadha. Kwanza kabisa, yametuwekea wazi dhana ya mielekeo; muundo wa mielekeo; ujenzi wa mielekeo; pamoja na muundo wa mielekeo. Pili, swala la mielekeo ya lugha, ikiwa ni pamoja na sababu mbalimbali zinazozua mielekeo tofauti kuhusu lugha mbalimbali katika jamii zimebainishwa. Tatu, umuhimu wa dhana ya mielekeo, pamoja na ukweli kuwa ni eneo ambalo limewashughulisha watafiti wengi, haswa katika taaluma ya saikolojia jamii na isimujamii imefafanuliwa. Aidha makala yametoa ripoti kuhusu utafiti mahsus kwa kuzingatia mbinu zilizotumika kuufanikisha utafiti huo pamoja na uchunguzi wa matokeo ya utafiti huo. Inafurahisha kugundua kwamba kuna matumaini kuhusu hali na



hadhi ya lugha ya Kiswahili kwani kinyume na makisio ya wengi mieleko ya wanafunzi katika mikoa miwili iliyotafitiwa ni chanya. Iwapo awali watu mkoani Nyanza walikichukia na kukidharau Kiswahili, kizazi cha sasa kinadhihirisha mtazamo tofauti kabisa

### Marejeo

- Ajzen, I. na Fishbein, M. (1980), *Understanding Attitudes and predicting Social Behavior*. Prentice-Hall, Inc., Eaglewood Cliffs, New Jersey.
- Bourhis, R.Y. (1982), "Language Policies and Language Attitudes: Le Monde De La Francophonie", katika: Ryan, E.B. & Giles, H. (1982) (whr.), *Attitudes Towards language Variation, Social and Applied Contexts*. Edward Arnold, London. pp. 34-62.
- Carranza, M. A. (1982), "Attitudinal Research on Hispanic Language Varieties", katika: Ryan, E.B. & Giles, H. (1982) (whr.), *Attitudes Towards Language Variation, Social and Applied Contexts*, Edward Arnold, London. pp. 63-83.
- Edwards, J. (1985), *Language, Society and Identity*, Basil Blackwell, Oxford.
- Edwards, J. R. (1982), "Language Attitudes and Their Implications Among English Speakers", katika: Ryan, E.B. & Giles, H.(1982) (whr.), *Attitudes Towards language Variation, Social and Applied Contexts*. Edward Arnold, London. pp. 20-33.
- Gorman, T.P. (1974), *"The Teaching of Languages at Secondary Level"*, katika: Whitely, W.H. (wh.), *Language in Kenya*. O.U.P., Nairobi.
- Holmes, J. (1992), *An Introduction to Sociolinguistics*. Longman, London and New York.
- Jahoda, M. & Warren, N. (wh.) (1966), *Attitudes*. Penguin Books.
- Kiesler, C.A., Collins, B.E., & Miller, N. (1969), *Attitude Change, A Critical Analysis of Theoretical Approaches*. John Willey & Sons Inc.
- Lemon, N. (1973), *Attitudes and Their Measurement*. B.T. Batsford Ltd., London.
- Odinga, O. (1967), *Not Yet Uhuru*. Heinemann, London.
- Okwany, A. (1995), "Attitudes of High School Students in Kenya Toward the Learning of Kiswahili." M.A., Thesis, University of New Brunswick, Canada.
- Onyango, J.O. (1990), "Mielekeo ya Wasomi Kuhusu Matumizi ya Lugha ya Kiswahili Nchini Kenya." M.A. Thesis, Kenyatta University.
- Oppenheim, A.N. (1966), *Questionnaire Design and Attitude Measurement*, Heinemann, London.
- Ryan, E.B. & Giles, H. (1982) (wh.), *Attitudes Towards Language Variation, Social and Applied Contexts*. Edward Arnold, London.
- Ryan, E.B. (1980) "Language Attitudes: Social Meanings of Contrasting Speech Styles," katika: H. Giles, W.P. Robinson na P.M. Smith (whr.), *Language, Social Psychological Perspectives*, Pergamon Press Ltd. Oxford.
- Summers, G.F. (wh.) (1970), *Attitude Measurement*. Rand, MacNally & Co., U.S.A.
- Triandis, H.C. (1971), *Attitude and Attitude Chang*. John Wiley & Sons, Inc. New York.

MA  
 Kwanza  
 Chuo Kik  
 mmoja al  
 majira ya  
 kuwa hak  
 hiyo. Kid  
 yangu ali  
 semina ile  
 Hii ni k  
 kimenishi  
 kuyatoa v  
 kwa lugha  
 nilijua ku  
 mbalimba  
 kila wana  
 Na hawa h  
 walilalami  
 Tukio  
 mwenzang  
 ya kijiogr  
 mwishoni  
 na kwamb  
 kuwa kifik  
 waliguna r  
 Kiingereza  
 Tutare  
 kulihusisha  
 ya Jamhur  
 uhuru wa  
 kusambaza